

# Njia Bora ya Kufundisha

Meta | My Digital World

# Njia Bora ya Kufundisha Ana kwa Ana

Ili kuendesha mafunzo katika madarasa yako kwa urahisi, ni muhimu kufuata njia bora sahili ili kuhakikisha wanafunzi wako wana wakati mzuri katika masomo yao. Orodha ifuatayo itakusaidia kujiandaa kwa ajili ya somo na ujihisi jasiri zaidi.

## MATAYARISHO

**Zingatia Muda:** Unapojiandaa kwa somo, ni muhimu kuuchunga vizuri wakati ili usichelewe au kufupisha maudhui. Inapowezekana, tafuta mtu atakayekusaidia zingatia muda au utumie saa ya kukukumbusha wakati wa kila kipindi. Wanafunzi hawatafurahi kama utalazimika kufupisha maudhui kwa sababu ya kuishiwa na muda. Pia, kuwa na Kitenda mbali cha kubadilisha slaidi zako ni muhimu ili kukusaidia kutoka kwenda mbele na kurudi nyuma katika kompyuta mpakato yako.

**Fanya Mazoezi:** Huhitaji kukariri slaidi za wasilisho, lakini unatakiwa kufanya mazoezi angalau siku 2-3 kabla ya kuziwasilisha ili kuhakikisha kwamba unakikumbuka kila kitu vizuri akilini mwako.

**Vaa Mavazi ya Kustarehesha na Yanayofaa Kwa Shughuli Hii:** Vaa viatu vinavyokustarehesha, hususan unaposimama kwa muda mrefu. Ili kuepuka kuhisi joto sana unapowasilisha, vaa mavazi juu ya mengine ambayo unaweza kutoa unapohitaji, kama vile jaketi na usivae nguo zinazobana.

**Maji:** Kuwa na chupa ya maji karibu yako kila wakati ili uwe na suluhisho la haraka ikiwa koo yako itakauka au ukikohoa.

## LUGHA YA MWILI

**Kuwatazama Wanafunzi:** Hii humfanya kila mtu kujihisi ni wa kipekee na kujua kwamba umemuona. Hakikisha unazungusha macho yako kwenye chumba kizima na huangalii mtu mmoja tu. Epuka kuangalia sana skrini ya maonesho. Hii mara nyingi inamaanisha kwamba utawapa mgongo wanafunzi wako, jambo ambalo sio zuri. Pia inamaanisha kwamba sauti yako inaelekea upande usiofaa. Ikiwa unanyoosha mkono kuonyesha kitu kilicho kwenye skrini, unatakiwa kusimama kwa kuwaelekea wanafunzi wako huku mkono wako ukielekeza macho yao kwenye sehemu wanayotakiwa kutazama.

**Tabasamu:** Kila wakati kumbuka kutabasamu. Inasaidia watu kustarehe, kuwapa furaha na kuwahimiza waone raha.

**Kusogeza Mikono:** Jaribu na uepuke kutumia sana mikono kwa sababu hili huvuruga kile unachokisema. Jaribu kutumia mikono wakati unapoeleza jambo fulani kwenye slaidi ili kusaidia kuwaonesha wanafunzi taarifa fulani iliyo kwenye skrini. Epuka kutapatapisha mikono yako bila sababu kwa kuwa hilo hukufanya kuonekana kana kwamba una wasiwasi. Kama wewe huchezesha mikono yako sana, jaribu kushika chupa ya maji. Hii itakusaidia kuacha kuchezesha mikono yako sana.

# Njia Bora ya Kufundisha Ana kwa Ana

## KUWASILISHA

**Shirikisha Darasa:** Kila unapoweza, waulize wanafunzi maswali. Kufanya hivyo hakukupi tu muda wa mapumziko unapoongea lakini pia huwafanya wanafunzi kushiriki na kutafakari. Pia unaweza kuwa na vitafunio vidogo vya kupatiana wakati mwanafunzi anapotoa jibu sahihi.

**Zungumza kwa Ufupi:** Yaweke maelezo yako kwa ufupi na wazi. Kadri unavyoongeza maneno, ndivyo watu watakavyokosa kupata ujumbe wa msingi. Maelezo mafupi na wazi ndiyo siri ya mafanikio.

**Kasi ya Maongezi:** Jaribu usizungumze kwa haraka sana. Hii itakufanya kuonekana kana kwamba una wasiwasi na watu hawataweza kufuatilia unachosema. Punguza kasi yako na uvute pumzi kama kawaida.

**Makadirio:** Zungumza kwa sauti ya juu na kwa wazi. Epuka kuweka mikono yako kwenye kinywa chako, usiangalie chini kwenye sakafu na uzungumze kwa sauti yenye ukakamavu.

**Ongeza Zoezi:** Ili kusaidia kuweka mapumziko katika wasilisho na kuwashirikisha wanafunzi, jaribu kuongeza zoezi.

**Weka Ucheshi:** Ukiwachekesha watu kidogo, inawezekana kwamba wanafunzi watafurahia somo hilo zaidi.

**Hakuna Lugha Chafu:** Usijiingize katika hatari ya kutumia lugha chafu kwa sababu hilo huenda likawachukiza watu wengine. Kutotumia maneno machafu hakutamuudhi mtu yeyote.

## ENEO LA MAFUNZO

**Fahamu Eneo Utakapowasilisha:** Ikiwa huwasilishi katika mazingira ya darasa la kawaida, jaribu kutembelea eneo hilo kabla ya kuwasilisha. Ni muhimu kufanya hivyo ili usichelewe na uwe tayari katika siku ya kuwasilisha na usikumbane na hali ambazo hukutarajia. Unahitaji kujua ni vifaa na nyenzo gani zinazotolewa, na ni vipi unavyotakiwa kuja navyo wewe. Shirikiana na msimamizi wa eneo la wasilisho ili kuhakikisha kwamba unafahamu mpangilio wa chumba hicho na umwambie kwa uwazi kuhusu vitu utakavyovitaka chumbani humo ili uendeshe somo lako vizuri.

Hakikisha una taarifa za mawasiliano ya mtu atakayewajibika eneo hilo siku ya somo lako — hakuna maana ya kumpigia mtu simu ambaye yuko mbali likizoni. Hii inaweza kuwa tofauti na mtu utakayewasiliana naye kwa masuala ya jumla ya eneo hilo, hivyo ni vizuri kuwa na maelezo ya mawasiliano ya watu hao wawili.

Ikiwa kuna vizuizi au vikwazo vyovyote katika eneo hilo, utahitaji kuwajulisha wanafunzi wako. Kwa mfano, eneo hilo na rasilimali zake zinaweza kufikiwa na watu wanaotumia viti vya magurudumu? Ni vizuri kuwajulisha wanafunzi wako mapema kuhusu masuala kama haya.

# Njia Bora ya Kufundisha Ana kwa Ana

**Fanyia Wasilisho Lako Majaribio:** Ni kwa vipi utakuwa unawasilisha slaidi za PowerPoint? Utakuwa unawasilisha moja kwa moja kutoka kwenye kipakatalishi chako hadi kwenye skrini au kutumia projekta hadi kwenye skrini? Je, kuna ubao mweusi au mweupe wenye kalamu zinazofaa za kuandikia dondoo au chati mgeuzo?

Hakikisha kwamba skrini yako inaonesha picha katika fomati ya 16:9 yaani kwa mkao kama wa karatasi ya A4, na sio kama projekta zingine za zamani zilizoonesha picha kwa fomati ya 6:6.

Unapotembelea eneo la wasilisho au darasa, beba kipakatalishi chako kilicho na sampuli ya slaidi za PowerPoint ili ufanye jaribio la wasilisho. Kufanya hivyo kutaonesha matatizo yoyote, ili uweze kuyatatua.

**Vyoo viko Wapi:** Kabla ya somo, angalia vyoo viko wapi, ni vingapi, ikiwa vinatumiwa na watu wa jinsia zote na kama vinaweza kufikiwa na watu wote.

**Mambo ya Kufanya na Kutofanya Katika Eneo la Wasilisho:**

*Fanya:*

- Kuwa na jina na namba ya simu ya mwakilishi wa eneo la wasilisho aliye katika zamu, ili uwasiliane naye ikiwa utahitaji usaidizi.
- Zunguka kwenye eneo hilo na katika chumba cha mawasilisho ili kuhakikisha kila kitu kiko sawa.
- Unganisha kompyuta yako ili kuhakikisha kwamba sauti na picha zinafanya kazi vizuri.

*Usifanye:*

- Kufika katika siku ya wasilisho bila kutembelea eneo hilo hapo kabla!
- Kupuuza chochote: fika ukiwa umejitayarisha na ubebe kila kitu ambacho huenda utahitaji ikiwa ni pamoja na vitini, nyaya, spika na betri.

## MIONGOZO YA KUFANYA MAWASILISHO

*Kabla ya Mawasilisho*

- **Matayarisho na Utafiti:** Fanya mazoezi ya maudhui ya wasilisho angalau siku 2-3 kabla ya kuwasilisha ili uyafahamu na uyaelewe vizuri. Kufanya hivyo kutakupa muda wa kufanya utafiti kuhusu maswali au hoja mpya utakazopata.
- **Ukubwa wa Darasa/Wanafunzi:** Fahamu ni wanafunzi wangapi watakaokuja ili chumba kitayarishwe ipasavyo. Fikiria kuhusu jinsi ya kuhusisha hadhira yako vizuri zaidi ukizingatia ukubwa wa hadhira unayotarajia.
- **Vitu Utakavyobeba:** Baada ya kutembelea eneo la wasilisho, andika orodha ya vitu utakavyobeba ili kuhakikisha somo linafanyika vizuri. Pia tunapendekeza kwamba unakili slaidi zote kwenye diski mweko, ili uwe tayari kwa hali zozote!

# Njia Bora ya Kufundisha Ana kwa Ana

### *Wakati wa Wasilisho*

- **Zingatia Muda:** Tumia mfumo wa kompyuta yako wa kupima wakati, saa, simu ya mkononi au saa ya ukutani ili kuhakikisha kwamba unafuata ratiba na una wakati wa kufundisha maudhui yote.
- **Soma Hadhira Yako:** Kutakuwa na nyakati ambapo umakinifu wa wanafunzi wako utavurugika au uwape maarifa mengi kiasi kwamba watazidiwa, kwa hivyo kuwa makini wakati unapotaka kuwachangamsha kwa maongezi ya kuwapunguzia mawazo au mapumziko mafupi. Hili litatumika kwako pia. Ikiwa utahisi kana kwamba nguvu yako inapungua, chukua mapumziko mafupi au uwashirikishe wanafunzi wako katika shughuli fulani au mjadala.
- **Kuwa Mchangamfu:** Kuzungumza kwa saa chache kunaweza kuchosha, lakini ni muhimu kwamba unabaki ukiwa na nguvu na mchangamfu katika somo lote.

### *Baada ya Wasilisho*

- **Maswali na Majibu:** Toa muda wa vipindi vya Maswali na Majibu. Vinaweza kuwa vifupi na viwe mwishoni mwa kila kipindi. Ikiwa utaulizwa swali ambalo huwezi kujibu, andika swali hilo na ulijibu baadaye kupitia barua pepe. Sio kosa kusema hujui jibu la swali fulani. Usijaribu kubuni jibu ambalo haliendani na mtazamo wa Meta.

# Njia Bora ya Kufundisha kwa Njia ya Mtandao

Kuwashirikisha wanafunzi katika masomo ya mtandaoni kunahitaji ubunifu mkubwa, uchangamfu na kuandaa masomo kwa njia mahususi. *Unafahamu maudhui yako na jinsi ya kuyafundisha kwa wanafunzi.* Kwa matayarisho na mawasilisho mazuri kupitia somo la mtandaoni, unaweza kuwashirikisha kwa njia nzuri na kupata matokeo mazuri. Mapendekezo yaliyoko hapa chini yatakusaidia unapohamia katika masomo ya mtandaoni au yale yanayochanganya masomo ya mtandaoni na ya ana kwa ana, na kukusaidia kukuza ujuzi, ukakamavu, na uwezo wako wa kufundisha mtandaoni kwa njia nzuri. Ikiwa wewe ni mgeni kwa masomo ya mtandaoni au una tajriba kama mkufunzi wa mtandaoni, Mazoea bora yafuatayo yanaweza kukusaidia katika safari yako ya kuwa mkufunzi mzuri, bila kujali pahali unapofundisha.

## KUPANGA DARASA LAKO

**Kumbuka Mambo Muhimu:** *Kuwafahamu wanafunzi wako na jinsi wanavyosoma ni muhimu kwa masomo ya mtandaoni sawia na ilivyo kwa masomo ya ana kwa ana.* Maudhui yanayoshirikisha hadhira, taratibu nzuri za kutoa mafunzo, usimamizi wa darasa na tathmini za mara kwa mara pia ni muhimu kwa masomo katika mazingira yote. Kadri unavyotengeneza mtaala wako, masomo na shughuli za masomo ya mtandaoni, zingatia jinsi utakavyoweka mipango ya kila kipengele cha mafunzo bora kwa namna sahihi na ya usawa, jinsi vitavyotakiwa kutofautiana katika masomo ya mtandaoni na jinsi utakavyovitumia kwa namna ambayo inatilia mkazo masomo ya wanafunzi na ufanisi wa kila mwanafunzi.

**Kuamua Kuhusu Muundo na Teknolojia:** Jiulize maswali yafuatayo ili kubaini ni muundo gani wa masomo na teknolojia inayofaa zaidi kwa darasa lako:

- Lengo la somo lako ni lipi?
- Je, linahitaji kuwashirikisha wanafunzi?
- Ni wanafunzi wangapi watakaohudhuria somo lako?
- Je, wanafunzi wako wanataka kuingia na kushiriki katika somo la mtandaoni linalopeperushwa moja kwa moja, au somo lililorekodiwa wanaloweza kutazama kila wanapohitaji?
- Je, kutakuwa na mwalimu zaidi ya mmoja?
- Je, wanafunzi watatumia kifaa gani ili kuliona somo: kipakatalishi au simu ya mkononi?
- Somo litadumu kwa muda gani?
- Je, wanafunzi wanatakiwa kuona maelezo yaliyo kwenye skrini, kama vile mipangilio na utendaji, au somo ni la nadharia tu?

# Njia Bora ya Kufundisha kwa Njia ya Mtandao

Sawia na mambo mengine, kuna manufaa na matatizo ya kila muundo, lakini maelezo yafuatayo yatakusaidia kubaini muundo unaofaa zaidi kulingana na malengo yako.

- Mafundisho yanayopeperushwa moja kwa moja kama vile semina ya mtandaoni au tukio linalopeperushwa moja kwa moja kupitia Facebook:
  - **Faida:** Mashirikiano ya papo hapo na wanafunzi, ukuzaji wa jamii wenye maoni ya papo hapo, na masomo yanaweza kuendelea kwa muda mrefu na bado yaendelee kusisimua wahusika.
  - **Matatizo:** Wanafunzi hawawezi kutazama somo hilo tena au kulisimamisha na kuliendeleza huku wakikamilisha shughuli zingine. Ikiwa kutatokea tatizo kama vile hitilafu ya intaneti au sauti, wanaotazama moja kwa moja watalishuhudia.

- Masomo unayoweza kupata kila unapoyahitaji kama vile video, sauti zilizorekodiwa, slaidi zenye sauti na masomo ya mtandaoni:
  - **Faida:** Masomo unayoweza kupata kila unapoyahitaji yanaweza kusasishwa. Unaweza kuhariri somo kabla ya kulitoa kwa wanafunzi. Wanafunzi wanaweza kuzipata nyenzo za masomo wakati wowote, kuzitama tena au kuanzisha na kusimamisha somo wanapokamilisha shughuli zingine.
  - **Matatizo:** Hakuna maingiliano ya moja kwa moja ya kipindi cha maswali na majibu. Yanaweza kuhisi kana kwamba hayana ukaribu unaofaa na hayana sifa thabiti ya ukuzaji wa jamii. Mafundisho ya aina hii hayafai kwa masomo marefu, yaani ya zaidi ya dakika 40.

**Unapotengeneza masomo yanayoweza kufikiwa kila yanapohitajika, tafadhali hakikisha kwamba utapata idhini kutoka kwa Programu Meneja wa Meta wa eneo lako kabla ya kutoa somo ulilorekodi kwa umma.*

Unaporekodi masomo yanayoweza kufikiwa kila yanapohitajika, pia ni muhimu kuzingatia hadhira yako na pia ikiwa utakuwa unashughulikia watu wenye ulemavu wa kusikia. Kama ndiyo, basi tungependekeza uongeze tafsiri ya mazungumzo.

**Semina za Mtandaoni:** Unapochagua mfumo wa kuendeshea mkutano wa mtandaoni, ni muhimu kutafuta vipengele vitakavyowezesha muda mzuri wa mafundisho kwako wewe na pia kwa wanafunzi. Unapochagua mfumo utakaotumia, zingatia kama una vipengele vifuatavyo:

- Uwezo wa kuwa na nafasi ya wanafunzi wote watakaohudhuria, kwa mfano, ikiwa unataka kualika wanafunzi 100, angalia kama mfumo huo una nafasi ya idadi hiyo ya watu.
- Uwezo wa kutoa nafasi kwa masomo yasiyo na kikomo. Mifumo mingine hukuruhusu tu kuendesha masomo machache kabla ya kuanza kukutoza kwa kila somo la ziada.
- Hakuna kikomo cha maelekezo. Mifumo mingine huweka kikomo cha muda wa mafundisho kisha masomo yanakatishwa.
- Hukuruhusu kuandika katika ubao wa mtandaoni, ili uweze kuangazia sehemu za skrini unazozungumzia, kuchora, n.k.
- Hukuruhusu kuvigawa vyumba ikiwa unataka kuwagawa wanafunzi katika makundi madogo ili kufanya shughuli fulani.
- Hukuruhusu kurekodi somo lako. Tafadhali hakikisha una idhini ya wanafunzi kabla ya masomo yanayorekodiwa na uzilinde siri za wanafunzi.
- Uwezo wa kuhakikisha kila mtu anaiona skrini, ili uoneshe slaidi, nyaraka, n.k.

**Vidokezo:**

1. Wape wanafunzi slaidi ya utangulizi inayoeleza utendaji wa mfumo wa mkutano wa video unaotumiwa ili wafahamu jinsi ya kuuliza maswali, kujibu maswali ya hojaji, ubao, n.k.
2. Usitumie slaidi zenye maelezo mengi sana, hasusan ikiwa wanafunzi wako wanatumia simu za mkononi kuingia kwenye mkutano. Slaidi zenye maelezo mengi zinaweza kuwa na matini nyingi, picha, grafu, video, n.k.
3. Ikiwezekana, pia kuwa na msimamizi kwenye somo. Msimamizi anaweza kujibu maswali yaliyo kwenye kidirisha cha gumzo, kuweka wakati na kuelekeza maswali kwa mwalimu. Ni vigumu kufanya haya yote huku ukiwasilisha kuhusu mada fulani peke yako.
4. Rekodi masomo ili uweze kurudi nyuma na kupitia maswali, n.k. Hii itakusaidia kuwa na mambo zaidi husika ya kusema unapotoa huduma anuwai za kusaidia wanafunzi na unapoendesha mijadala baada ya masomo. Kabla ya kurekodi somo fulani hakikisha kwamba umewajulisha wanafunzi kwamba somo litarekodiwa kabla ya kuanza — kulingana na sheria za siri za nchi yako huenda ukahitajika kupata idhini yao.
5. Mifumo mingine humruhusu anayeendesha mkutano ajumuishe hojaji na mazoezi kwenye masomo. Ikiwa hilo litawezekana, buni hojaji na mazoezi hayo kabla ya somo ili yawe tayari kutumika yanapohitajika.
6. Hakikisha kwamba umezima maikrofoni za wanafunzi wote, ili usivurugwe mawazo na kelele wakati somo linapoendelea. Wanafunzi wanaweza kuwasha maikrofoni zao ikiwa wanataka kuuliza swali.

**Mafundisho Yaliyorekodiwa Kabla:** Masomo ya video/sauti yaliyorekodiwa ni njia nzuri ya kufikisha masomo kwa wanafunzi wengi. Baada ya kumaliza kurekodi na umeridhika na matokeo, unaweza kuyasambaza kupitia mifumo mbalimbali na mara kwa mara. Manufaa mengine kwa mwanafunzi ni kwamba anaweza kutazama somo zaidi ya mara moja, na anaweza kusitisha na kuendelea na somo lililorekodiwa huku akikamilisha kazi zingine.

Jambo zuri zaidi kuhusu kurekodi video/sauti ni kwamba ni sawa kufanya makosa. Unaweza kusitisha na kurekodi tena mara nyingi kadri inavyotakiwa. Ni rahisi zaidi kutengeneza video/sauti ya kitaalamu ikilinganishwa na kutoa hoja hizo za kitaalamu moja kwa moja, lakini kama ilivyotajwa hapo awali, kila hali ina manufaa/matatizo yake.

Manufaa ya video iliyorekodiwa inayotazamwa kwa simu ni kwamba mwanafunzi anaweza kugeuza mkao wa simu yake na aone mambo yanayowasilishwa katika skrini kubwa zaidi.

**Vidokezo:**

1. Kutumia mfumo wa mkutano wa mtandaoni ni njia nzuri ya kurekodi somo lako. Unaweza kuanzisha mkutano wewe tu kisha utumie huduma za kuhakikisha kila mtu anaiona skrini, ubao na kurekodi ili kurekodi somo lako. Faili hiyo kisha inahifadhiwa katika muundo wa MP4 na ni rahisi kuishiriki na wanafunzi wako.
2. Utakapobonyeza kitufe cha kuanza, hesabu hadi tatu kabla ya kuanza kuzungumza. Sawia na hilo, mwisho, hesabu hadi tatu kabla ya kubonyeza kitufe cha kusimamisha.

# Njia Bora ya Kufundisha kwa Njia ya Mtandao


## FACEBOOK LIVE

Facebook Live ni mfumo mzuri sana wa kutumia ili kuamiliana na wanafunzi wako na ni njia nzuri ya kuzungumza nao moja kwa moja. Jibu maswali yao, sikiliza maoni waliyonayo na uangalie ishara za miili yao ili kujua jinsi darasa lako linavyoendelea. Wanafunzi wako wanaweza kupokea arifa utakapoanzisha mkutano, ili wajiunge na somo lako katika wakati unaofaa.

Facebook Live pia huwaonesha wanafunzi wako yanayoendelea mambo yanayohusika katika uandalizi wa masomo na kuwapa fursa ya kuamiliana nawe bila vikwazo kuhusu maudhui ya somo lako.

**Vidokezo:**

1. Ubora wa muunganisho wako wa intaneti hubaini ubora wa muda wako na wa hadhira. Ukipima kasi katika wakati fulani wa siku, huenda ikawa tofauti katika wakati mwingine. Muda mbaya zaidi ni kati ya saa 11 alasiri na saa 2 usiku, Kumbuka: Facebook Live hupendekeza kiwango cha biti kisichozidi kilobiti 4000 (4 mbps) na kiwango cha biti cha sauti kiwe 96 Kbps au 128 Kbps.
2. Ili kuanza kutumia Facebook Live, tunapendekeza utazame viungo vilivyo hapa chini:
    - Vidokezo vya kuendesha mapeperusho ya Facebook Live
    - Jinsi ya kuanzisha mapeperusho ya Facebook Live
    - Jinsi ya kuratibu mapeperusho ya Facebook Live
3. Kumbuka kwamba kuna uwezekano mkubwa kuwa wanafunzi wataingia kupitia simu ya mkononi — picha ifuatayo inaonesha skrini wanayoweza kutarajia kuona.



4. Ratibu mkutano wako wa Facebook Live kama tukio linalohamasisha wanafunzi wako au katika Kundi la Facebook.

# Njia Bora ya Kufundisha kwa Njia ya Mtandao

**Tengeneza Mandhari:** Utakapowasha kamera yako, unawasha taa darasani mwako; fikiria kuhusu mandhari unayotaka kuweka. Weka usuli utakaojaliza somo lako na kumakinisha au kuchangamsha wanafunzi wako (kulingana na mahitaji yao). Ukuta wenye rangi moja ulio na ujumbe wa kutia motisha au wito wa kila siku uliondikwa kwenye karatasi na kubandikwa, rafu sahili ya vitabu itakayomakinisha wanafunzi katika mazingira ya masomo, au usuli wa Zoom wa maabara ya kisayansi ni mifano ya jinsi unavyoweza kutengeneza mandhari yako ili kulingana na nia na masomo yako. Pia unaweza kuweka vitu kama mimea/picha kwenye ukuta au usuli ili uwe na mandhari anuwai zaidi. Jaribu usiweke vitu vingi sana kwenye picha. Epuka kuta zilizopigwa ruwaza, samani zisizohitajika, au vitu vingi vilivyotapakaa kwenye chumba. Usuli mtulivu wenye rangi iliyofifia, rangi zisizotofautiana sana na rangi nyororo mara nyingi huwa usuli mzuri zaidi. Hakikisha una nafasi ya kutosha ili uwe umbali mzuri kutoka kwenye kamera.

Waoneshe wanafunzi wako kwamba umejitolea kuwapa kiwango cha umakinifu na kujitolea, sawia na kiwango unachotaka kutoka kwao. Punguza kuvurugika kwa akili kwa kutengeneza sehemu yako ya kazi katika eneo la nyumba yako lisilopitwa na watu wengi na uweke simu za mkononi au vitu vingine vinavyovuruga akili mbali sawia na jinsi ungefanya katika darasa halisi — hata ikiwa vitu hivyo havionekani kwenye skrini.

**Onekana:** Mawasiliano na masomo huendeshwa kwa njia mbalimbali; kwa kuwa hauko katika eneo moja na wanafunzi wako hakumaanishi kwamba huna mawasiliano halisi na wanafunzi wako. Utataka kuonekana vizuri ili nyote mnufaike kutoka kwa sifa zote za mawasiliano ili kusaidia katika masomo na maamiliano, kutoka kwa ishara za uso katika masomo ya lugha hadi tabasamu la furaha na fahari kwa sababu ya ufanisi wa mwanafunzi. Kaa katika sehemu iliyo mraba kutoka kwa kamera, huku ukihakikisha kwamba uelekeo wa macho yako uko sawa na uelekeo wa kamera kadri inavyowezekana. Unapoweka kifaa chako ili kurekodi, hakikisha kwamba unaacha nafasi katika sehemu ya juu, ili kichwa chake kisiwe juu kabisa kwenye skrini. Fuata agizo la kugawa picha kwa thuluthi ili picha iwe na usawa unaofaa. Epuka kuvaa shati na marinda yenye mistari, alama ndogo au mistari mieusi na mieupe kwa sababu mavazi haya hayatapendeza kwenye video. Mwanga wa asili ndio unaofaa zaidi kwa kurekodi video na kupiga picha. Ikiwa chanzo chako cha mwanga kiko nyuma au juu yako, mwanga utang'aa juu yako na kufanya uwe na duara leusi chini ya macho yako. Hili litakufanya uonekane kama mtu asiyeaminika. Hivi hapa ni vidokezo zaidi vitakavyokusaidia:

- Unatakiwa kuelekea kwenye mwanga, lakini mwanga usiwe mkali sana kiasi kwamba unafunga macho kidogo.
- Chanzo cha mwanga kinafaa kutoka nyuma ya kamera.
- Ikiwa hakuna mwanga wa asili, na unatumia taa zilizo kwenye dari, zitatoa mwanga mzuri kwenye nyumba lakini hakikisha kwamba hujasimama moja kwa moja chini ya taa kwa kuwa hilo litasababisha vivuli.
- Tumia taa ya mezani au tochi isiyo na mwanga mkali inayokumulika ili kuweka sawa mwanga. Kadri taa hiyo itakavyokuwa mbali na wewe, ndivyo mwanga wako utakavyokuwa wa kawaida kwenye uso wako.
- Mwanga mdogo unaomulika uso wako na kamera inafaa kuwa katika kiwango sawa na macho yako.

**Sikika:** Sauti ya kutegemewa na yenye nguvu ni muhimu katika kumakinisha wanafunzi na kuboresha mafundisho yao. Masomo ya mtandaoni hutegemea mafundisho ambapo mkufunzi hayuko kwenye skrini au haonekani. Hii husasan huonekana unapohakikisha kila mtu anaiona skrini au vitu vilivyomo. Katika nyakati hizi, toni ya sauti imara na changamfu huwa muhimu sana. Ishara za sauti zinaweza kueleza mambo ambayo hapo kabla ungetegemea tu ishara za mwili au mbinu zingine za mazungumzo zisizotumia maneno ili kuelezea, katika hali ya kawaida. Kumbuka kuwatia moyo wanafunzi wako kwa sauti ya juu, kwa kuwa huenda hawataweza kuona ukiamkia kwa kichwa chako au kutabasamu kama njia ya kuwatia moyo.

# Njia Bora ya Kufundisha kwa Njia ya Mtandao

**Wafundishe Wanafunzi Wako Teknolojia:** Kumbuka kwamba, kama ulivyo wewe, huenda pia wanafunzi wako ni wageni kwa masomo ya mtandaoni. Baada yako kuwa na fursa ya kubaini na kujifunza mazoea bora ya kujifunza mtandaoni, hakikisha umewapa wanafunzi wako maarifa yako kama somo lako la kwanza la mtandaoni. Ikiwa somo hili ni la kutoa maarifa au ndilo somo la kwanza pamoja, hakikisha kwamba wanafunzi wako wanafahamu jinsi ya kutumia mbinu na zana zote, pahali watakapopata nyenzo na kuelewa matarajio yako kuhusu kuhudhuria na kushiriki kwao. Hakikisha kwamba wazazi/walezi/waangalizi wamealikwa ili kujifunza kuhusu teknolojia hiyo na kufahamu matarajio pia.

**Orodha Yako ya Ukaguzi ya Vifaa:** Kwa kuwa husafiri, hilo halimaanishi kwamba huendi kazini. Kusanya nyenzo unazohitaji kwa ajili ya shughuli za siku hiyo na uzipeleke kwenye eneo utakalofanyia kazi. Hii ni pamoja na zana na nyenzo zitakazotumika — kama vile chaja, penseli, karatasi na vitabu — pamoja na bidhaa za kujistarehesha kama maji, vitafunwa na shashi.

Sawa na hilo, waandikie wanafunzi wako orodha ya bidhaa ambazo zitawasaidia na/au ni muhimu kwao kuweka karibu na uwape orodha hiyo kabla ya somo. Hii itahakikisha kwamba wanafunzi wako wote wanaweza kupata bidhaa zozote zinazohitajika ili kushiriki katika masomo kikamilifu, kuwa na muda wa kutosha wa kusema ikiwa hawatapata bidhaa hizo ili mipango mbadala ifanywe na kwamba mara baada ya somo kuanza, hakuna wakati utakaopotezwa huku wanafunzi wakikimbia kwenye chumba kingine kuchukua daftari.

## KUTUMIA ZANA ZAKO

**Fanya Majaribio ya Maikrofoni:** Kuendesha somo linalopeperushwa moja kwa moja au lililorekodiwa hufanyika vizuri zaidi kwa kutumia kisikizi kizuri chenye maikrofoni na katika mazingira yenye ukimya. Ikiwa una nafasi au unapenda kutembeatembea, tumia kifaa cha maikrofoni na kisikizi kisicho na waya ili sauti yako ibaki sawa hata kama umesimama ili kueleza sehemu fulani ya somo. Kabla ya kuanza somo au kuanza kurekodi, fanyia vifaa vyako majaribio katika eneo utakalotumia ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wataweza kukusikia moja kwa moja, kwamba hakutakuwa na miangwi au usumbufu usiotarajiwa na kwamba faili unazorekodi zinasikika vizuri na ni rahisi kuelewa.

**Fanya Mazoezi ya Kutumia Mfumo Wako:** Tenga muda wa kufanya mazoezi ya kutumia mfumo wa masomo ya mtandaoni na kufanya marekebisho yoyote yanayohitajika. Hakikisha kwamba kimo cha kamera/kompyuta yako kitawezesha kuonekana vizuri kwa sura yako na kwamba maikrofoni yako imewekwa katika pahali ambapo inanasa sauti yako vizuri zaidi. Chukua muda wa kuhakikisha una ufahamu mzuri wa kuzungumza kwenye kamera, kutumia mfumo wa kuwasilisha na kubadilisha kati ya skrini ya mapeperusho ya moja kwa moja na slaidi, video na zana zingine. Pia unaweza kurekodi masomo yako (hata ikiwa unafundisha moja kwa moja) ili uyapitie baadaye na utambue sehemu zinazohitaji kuboreshwa kwa maudhui na uendeshaji wa mafundisho.

**Kagua Kabla ya Kuanza:** Ikiwa unarekodi somo, hakikisha kwamba una nafasi ya kutosha kwenye simu/kipakatalishi chako ya kuhifadhi faili hiyo. Hifadhi picha na video zako katika kifaa kingine ili kutengeneza nafasi, kama itahitajika. Ikiwa unapeperusha moja kwa moja, basi inapendekezwa sana kwamba upime kasi ya muunganisho wako wa intaneti. Hakikisha una soketi ya umeme karibu yako utakayotumia.

**Ondoa Vizuizi vya Ufikiaji:** Mifumo mingi ya mikutano na mafundisho ya video ina mipangilio ya tafsiri ya mazungumzo, kubadilisha matini kuwa sauti au zana zingine zilizo ndani ya mifumo hiyo za kusaidia wanafunzi kwa mahitaji tofauti ya ufikiaji. Angalia machaguo yaliyopo kwenye mfumo wako ili uwasaidie wanafunzi wako kuyawezesha.

# Njia Bora ya Kufundisha kwa Njia ya Mtandao

**Jiandae kwa Ajili ya Hitilafu za Teknolojia:** Ikiwa wanafunzi wako watakuwa na tatizo la kuunganishwa, ni vyema kuwa na hifadhi ya shughuli huru na masomo yaliyorekodiwa, au yasiyo ya moja kwa moja yaliyotengenezwa ambayo yanaweza kutumika kwa urahisi ikiwa kutatokea hitilafu za miunganisho au teknolojia. Video fupi zilizorekodiwa kabla, mafundisho au mazoezi ya kasi yanayohusiana na somo hilo, au nyenzo zingine ambazo wanafunzi wanaweza kutumia katika hali ambapo hitilafu itatokea zitahakikisha kwamba hakuna muda wa masomo utakaopotezwa huku wanafunzi wakisubiri hitilafu hiyo itatuliwe na kwamba wanafunzi watamakinika katika somo. Unaweza kufikiria kutengeneza mkusanyiko wa shughuli sahili zisizo za mtandaoni ambazo wanafunzi wanaweza kujishughulisha nazo ikiwa hamuwezi kuwasiliana kupitia mtandao. Tengeneza melekezo mepesi yanayoweza kufuatwa na wanafunzi, kama vile zoezi la kusoma la dakika 20 au mchezo wa kutafuta na kukusanya vifaa vya nyumbani.

Hakikisha kwamba wanafunzi wana orodha ya shughuli na maelekezo hayo kabla ya hitilafu yoyote kutokea; kwa mfano, kwa kuyasambaza kabla kupitia barua pepe pamoja na mpango wa somo wa kila siku au juma na nyenzo zingine. Katika somo lako la kwanza kuhusu teknolojia, wafundishe wanafunzi wako kuhusu wanachotakiwa kufanya ikiwa watapoteza muunganisho kabisa au kwa kiwango fulani, na urudie utaratibu huu mara kwa mara ili wawe tayari, ili usijikute ukijaribu kufikiria jinsi ya kuwapa maelekezo huku ukijaribu kutatua hitilafu hiyo.

## KUBORESHA MASOMO YAKO

**Kuwa na Mapumziko Katikati mwa Masomo:** Masomo na maamiliano ya mtandaoni yanahitaji kiwango cha juu cha utendaji wa akili na kiasi kwamba unatakiwa kupanga kwa makini kuhusu jinsi ya kuwasilisha masomo yatakayowachosha — au kuwachanganya kabisa — wanafunzi wako. Kumbuka kwamba, kwa wanafunzi wengine, hawajifunzi masomo hayo tu bali pia kuhusu teknolojia na zana na jinsi ya kuzitumia. Panga masomo, yaliyo na/au yasiyo ya moja kwa moja, katika vipindi vidogo vidogo ili kuongeza maamiliano na kudumisha umakinifu. Badilisha kutoka kwenye shughuli za kutumia nguvu nyingi na kidogo, na ujumuishe mapumziko ya kutuliza akili na ya kusogeza mwili.

**Tumia Ubao:** Chukulia skrini kama ubao mweupe au skrini janja, na ujumuishe matumizi yake kwenye somo lako ili kutilia mkazo hoja kwa kutoa muktadha, kuashiria kazi na kuonesha mifano jinsi ambavyo ungefanya katika darasa halisi. Unapofundisha kupitia mtandao, zingatia mbinu unazoweza kutumia skrini ili kuweka fremu kwenye hoja unazofundisha. Tumia zana za ufafanuzi, kama vile mishale na kuchora mistari, ili kuonesha maendeleo na kusaidia kutoa mawazo. Waalike wanafunzi wako kwenye ubao ili waongoze au kulionesha darasa kitu fulani.

**Chagua Mchanganyiko Wako:** Unapopanga masomo yako, amua ni sehemu zipi zitakazowasilishwa ana kwa ana na/au kupitia majadiliano katika skrini, video iliyorekodiwa kabla au video ya mhusika wa tatu, slaidi za wasilisho/matini zinazooneshwa kwenye skrini, na kazi huru. Kubadilisha jinsi unavyowasilisha taarifa na kuwaomba wanafunzi wajibu kunaweza kuongeza maamiliano na kumbukumbu. Zingatia ni zana zipi za mtandaoni ambazo utahitaji wewe pamoja na zile wanafunzi watakazohitaji, kama vile penseli, karatasi, au ubao unaofutika. Unapobuni muda huru wa masomo na mazoezi ya wanafunzi wako, kumbuka kubuni shughuli ambazo hazihitaji usaidizi mwingi kutoka kwa watu wazima au watu wengine walio nyumbani.

**Wahimize Waulize Maswali:** Masomo ya mtandaoni hutoa namna mbalimbali ambazo wanafunzi wanaweza kuuliza maswali kuhusu maudhui na nyenzo. Hii ina manufaa makubwa kwa wanafunzi ili wapate ufafanuzi wa kina kwa njia zinazolingana na mitindo yao ya masomo na viwango vinavyowaridhisha na ambavyo huenda havipatikani katika darasa halisi. Wafahamishe wanafunzi kuhusu njia tofauti wanazoweza kutumia kuuliza maswali (kwa maneno kwa sauti ya juu, kuyaandika kwenye kidirisha cha gumzo, kutumia kipengele cha mfumo cha "inua mkono" au kujumuisha shughuli ya swali wanalotaka kuuliza kwenye somo katika pahali ambapo wengine wanaweza kuongeza maswali yao kwenye ubao wa mtandaoni, kwa mfano).

# Njia Bora ya Kufundisha kwa Njia ya Mtandao

**Toa Mrejesho:** Walimu wana wajibu wa kusimamia na kufuatilia masomo. Tumia zana ulizo nazo na muundo wa masomo yako ili kutengeneza nafasi za kutoa maoni mara kwa mara kwa wanafunzi wako kuhusu kazi na masomo yao. Endesha mazoezi mafupi ya darasani na michezo ya mazoezi, na utumie mapumziko ya kujikumbusha mambo yaliyosomwa na vipindi vya kutathmini uelewa wa wanafunzi ili wanafunzi waelewe vizuri zaidi maudhui katika fomati tofuti. Toa mrejesho kwa maandishi kuhusu mazoezi yaliyowasilishwa na upange namna za kukusanya maoni ya wanafunzi kuhusu kazi za wanafunzi wengine inapohitajika. Tenga nafasi na wakati mahususi kwa wanafunzi ili ufuatilie maendeleo ya kila mmoja wao.

**Kushirikisha Jamii Yako:** Bila kujali muundo unaotumia kufundisha wanafunzi wako, ni muhimu kuzungumza na wanafunzi kabla na baada ya somo, ili waingiliane na somo hilo kwa namna anuawai, wala sio namna moja tu. Kutumia teknolojia kama vile Makundi ya Facebook, Makundi ya WhatsApp, mifumo ya mtandaoni ya mijadala au kwa kupiga simu kunamiliano na fursa ya kuendeleza mahusiano na wanafunzi wako. Pia, kutumia mchezo kama zoezi, jaribio la kutathmini uelewa au kazi ya nyumbani ni chaguo lingine unaloweza kutumia ili kuwashughulisha wanafunzi wako. Hii ni muhimu zaidi unapotoa masomo yanayofikiwa kila yanapohitajika kwa kuwa unahitaji kuwapa wanafunzi mfumo wa kujadili mada na kuuliza maswali. Mara nyingi, hii hujulikana kama maingiliano ya huduma anuwai za kusaidia wanafunzi.

Zungumza mara kwa mara na wanafuzni wako ili kuwafahamisha kuhusu masomo yajayo, jinsi ya kuuliza maswali, n.k. Lakini kuwa makini usiwasiliane nao mara nyingi sana au usiwape taarifa nyingi sana.

## KUTENGENEZA MANDHARI KAMILI YA DARASANI

**Anzisha Somo Imara:** Anza somo lako kwa kuwaruhusu wanafunzi wazungumze na wenzao. Hii hujenga mandhari huru na ya kirafiki na kuweka hali isiyo rasmi na ya kustarehesha ambayo itasaidia katika maamiliano ya wanafunzi, mashirikiano na kuwafanya wajisikie huru kuongea na kuuliza maswali. Weka ratiba au ajenda ambayo itaonekana vizuri katika kipindi cha mazungumzo ili wanafunzi wanaohitaji kufanya matayarisho kwa ajili ya somo waweze kuufahamu mpango vizuri na kwenye orodha hiyo, uweke bidhaa zozote ambazo wanafunzi watazihitaji katika somo hilo. Anzisha somo kwa zoezi la kuvuta pumzi, kuwatia moyo, kujaza shajara, ili kumakinisha wanafunzi na kuashiria kutoka kwenye mazungumzo baina yao hadi kwenye mazingira ya masomo. Hakikisha kuwa vipindi na shughuli hizi zitarudiwa katika kila somo, ili wanafunzi wajue watakachotarajia wanapoingia darasani.

**Wezesha Mahusiano ya Wanafunzi:** Katika masomo yako ya darasani kwako, buni namna zitakazowezesha maingiliano ya wanafunzi na waweze kusaidiana katika masomo yao. Watajifunza zaidi, na kufurahishwa na fursa ya kutoa mawazo pamoja, kushirikiana katika kazi za masomo na kufanya kazi hizo pamoja. Tumia hili pamoja na shughuli za masomo zilizobinafsishwa na masomo kamili ili kuwapa wanafunzi mafundisho kamilifu ambayo pia huboresha mahusiano na kujenga stadi za kijamii na za mashirikiano.

# Njia Bora ya Kufundisha kwa Njia ya Mtandao

**Jumuisha Masomo Yanayotumia Uzoefu:** Masomo yanayotumia uzoefu yanaweza kuwa zana ya kidijitali ya masomo sawia na yalivyo katika mafundisho ya ana kwa ana. Zingatia tatizo-, kazi-, huduma-, na mafundisho ya mtandaoni. Hii inaweza kufanywa kibinafsi, katika vikundi au kama darasa zima, na kuwapa wanafunzi masomo halisi na yanayoweza kutumika kote duniani ambayo yatatiliwa maanani na kusambazwa kwa darasa zima. Mifano ni kama:

- **Zoezi linalozingatia tatizo fulani:** Wape wanafunzi tatizo halisi katika jamii, kama vile mmomonyoko wa miamba, kisha uwaombe waliambie darasa zima kuhusu masuluhisho au mipango ya kutatua suala hilo.
- **Zoezi linalozingatia mradi fulani:** Waombe wanafunzi wapande mbegu za nyanya katika chungu na pia kwenye ardhi kisha wafuatilie ni mbegu zipi zitakazoota vizuri zaidi.
- **Zoezi linalozingatia huduma fulani:** Wape wanafunzi fursa ya kusomea wanafunzi wadogo kuliko wao kupitia mpango wa mtandaoni kubadilishana stadi na darasa lingine.
- **Mafundisho ya mtandaoni:** Tembelea ukumbi wa makumbusho unaoonesha midia bandia na za kielektroniki

**Fundisha Kuhusu Uraia wa Kidijitali:** Kuhamisha darasa kutoka kwa masomo ya darasani hadi kwa masomo ya mtandaoni ni fursa nzuri ya kufundisha, kutumia, kuboresha, na kukazia taratibu njema za uraia wa kidijitali kwa wanafunzi wako. Tumia darasa kama maabara yako, unaweza kuonesha na kufundisha wanafunzi jinsi ya kushiriki katika mazungumzo ya mtandaoni kwa heshima na uzingatifu kupitia gumzo na maoni, kutoa nyenzo nzuri kuhusu na kwa ajili ya maingiliano ya mtandaoni, na kuimarisha heshima ya utu na uwajibikaji kwa kwengine kupitia darasa hilo.

**Kujitunza/Kutunza Wengine:** Mafundisho na masomo ya mtandaoni yanaweza kuchosha na kutenganisha watu, hasa kama ni ya muda wote. Ni muhimu kufanya jitihada za kutengeneza namna za kukuwezesha wewe na wanafunzi wako kuwa na umoja, kujenga mahusiano, kujichangamsha na kuwa na raha ndani na nje ya masomo.

*Walimu ni wanachama wa jamii za masomo.* Kwa ajili yako, tafuta fursa za kuwa na mahusiano na walimu wengine katika jamii za mafunzo ya kitaalamu na za walimu wenza, ili kuwasilisha matatizo, kuzungumzia mambo mazuri pamoja na yanayokera, kushirikishana mipango ya masomo, nyenzo na vidokezo vya kufundisha. Hakikisha kwamba unajitunza — haijalishi kama ni kwa kufanya mazoezi mara kwa mara, kufanya shughuli inayokutuliza, au kuwa na muda mzuri na watu ulio na uhusiano wa karibu nao huku mkila — ili uingie darasani ukiwa na nguvu na bila mawazo mengi, na uwafundishe wanafunzi wako ipasavyo.

Katika madarasa yako, kuwa na vipindi vya mara kwa mara vya kusogeza viungo vya mwili na kwenda msalani. Tenga wakati ambapo wanafunzi watafurahia na kusherehekea pamoja, kusherehekea siku za kuzaliwa, mafanikio ya kipekee na likizo. Tengeneza mahusiano binafsi na wanafunzi wako, ukitumia muda wa kukutana na kila mmoja wao na kuzungumza nao kuhusu maisha yao, wala sio kazi zao tu.

**Tafakari:** *Walimu hufikiria kwa mpangilio mahususi kuhusu taratibu zao na kujifundisha kutoka katika mambo waliyopitia.* Mara nyingi, inaonekana kwamba fursa na nyenzo za masomo ya kidijitali hazina kikomo na ni nani aliye na wakati wa kujifundisha kuhusu zote? Jibu ni kwamba hakuna yeyote! Tafuta muda wa kutafakari kuhusu mikakati inayofanya kazi na mambo unayohitaji au yanayohitajiwa na wanafunzi wako. Kuwapa wanafunzi wako fursa za kutoa maoni ya haraka na yasiyo rasmi kuhusu masomo na zana mpya ambazo huenda unatumia kutakusaidia kukua kama jamii na kukuza desturi ya kufanya uchunguzi pamoja na kupenda masomo.

# Njia Bora ya Kufundisha kwa Njia ya Mtandao

**Nyenzo za Hiari:** Kuna nyenzo nyingi zilizo mtandaoni kwa ajili ya wakufunzi wanaoanza kuendesha mafundisho ya mtandaoni. Hizi hapa ni nyenzo nzuri unazoweza kuanza nazo.

Semina za mtandaoni kama vile msururu wa mafundisho ya Core Connection ya Bodi ya Kitaifa ya Viwango vya Mafundisho ya Kitaaluma, hutoa semina za mtandaoni kama vile Kila Kitu Unachotaka Kujua Kuhusu Teknolojia, ambayo itakufundisha kila kitu kuanzia jinsi ya kushiriki hati ya Google hadi jinsi ya kuweka picha yako juu ya usuli unaobadilika ili kutengeneza zana ya mafundisho inayopendeza (na kufurahisha) inayoashiria jinsi mafundisho ya stadi za kijamii na kihisia yanavyokuwa katika mazingira ya mtandaoni.

ISTE hutoa nyenzo nyingi bila malipo za masomo ya mtandaoni pamoja na kozi na mafundisho ya kitaaluma yaliyo mapana zaidi. Pia inatoa maelezo kuhusu taratibu nzuri za uraia wa kidijitali pamoja na namna za kusaidia wanafunzi wanaojifunza kuhusu uwanja huu.

Taasisi na mashirika mengi yamekusanya nyenzo za mafundisho mazuri ya mtandaoni na hutoa nyenzo zinazojumuisha katika masomo, pamoja na vyuo vikuu kama vile Chuo Kikuu cha Harvard na kampuni za vyombo vya habari kama PBS.

Kwa kawaida, walimu ndio nyenzo bora zaidi kwa maudhui yanayosambazwa! Wakufunzi kutoka kote ulimwenguni wanasambaza maandalio yao ya somo, kupitia mazoea bora na vidokezo vya kufundisha. Kujenga mahusiano na wakufunzi wenza, jamii za masomo ya kitaalamu, na mitandao ya wataalamu kutakupa mawazo mengi unayoweza kutumia kujenga, kupanua, kuboresha na kukuza kasi ya ukuaji wa taaluma yako!

*Bodi ya Kitaifa ya Viwango vya Mafundisho ya Kitaaluma ilichangia mwongozo huu. Ili kujifunza zaidi kuhusu shirika hili, tafadhali tembelea: nbpts.org.*

NATIONAL BOARD
*for Professional Teaching Standards®*